Jina la mtahiniwa: ……………………………………………………………………..

Saini: ……………………………………………………………………………...

336/1

LUGHA NA FASIHI

YA KISWAHILI

Saa 2

SHULE YA UPILI CLEVERLAND HIGHs

LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI

Karatasi ya Kwanza

(Insha na ufupisho)

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

Karatasi hii ina sehemu mbili, A na B.

Chagua swali moja kutoka kila sehemu

**SEHEMU A**

**INSHA**

Ama

1. Katika shule yako kumeanzishwa chama cha kuhifadhi mazingira na wewe ndiye mwenyekiti wa chama hicho. Majanga mengi hutokea kwa kukosa kuhifadhi mazingira vizuri. Wape wanafunzi wenzako ushauri kuhusu jinsi ya kuepukana na majanga.

Au

2. Wewe ni Afisa wa afya katika mtaa wenu, vijana wamejiingiza sana katika utumiaji wa dawa za kulevya na yamewaathiri vibaya sana. Umealikwa kuzungumza na vijana hawa katika jamii yako. Waeleze athari ya dawa za kulevya katika afya yao na jamii wanamoishi.

## SEHEMU B

## UFUPISHO

3. Soma taarifa uliopewa kisha uifupishe kwa kutumia maneno themanini ,(80).

## FAIDA YA SHEREHE ZA KITAIFA

Sherehe za kitaifa ni vitendo vya furaha vinavyofanywa na watu wengi ili kusherehekea matukio makubwa ya Kitaifa. Sherehe hizi hujumuisha viongozi wa ngazi mbali mbali wa kisiasa, viongozi wa kidini, viongozi wa kitamaduni na wengine.

Sherehe hizi zina kazi kubwa katika nchi. Zinatusaidia kukumbuka matukio muhimu ambayo yamewahi kutokea katika historia ya taifa letu.

Vile vile, sherehe zinasaidia vizazi wa kisasa (Generation Z) kutambua na kuwaenzi mashujaa wa zamani waliopigania uhuru na ukombozi wan chi fulani. Mashujaa kama mwenda zake Jomo Kenyatta, Dedan Kimathi, Julius Nyerere, Nelson Mandela, Robert Mugabe na wengine waliopigania uhuru na ukombozi wa mataifa ya Afrika.

Sherehe za Kitaifa husaidia katika utetezi wa wanyonge ambao wananyanyaswa na kukoseshwa haki zao. Kwa mfano, Siku ya Kimataifa ya Wanawake na siku ya Kimataifa ya Wafanyakazi, wanawake na wafanyakazi hutetewa. Sherehe hizi huimarisha umoja na ushirikiano wa Kitaifa. Hii ni kwa sababu wakati wa maadhimisho watu kutoka sehemu mbali mbali na makabila tofauti tofauti hukutana na jambo hili hukuza na kuimarisha upendo, uzalendo, mshikamano, maridhiano na ushirikiano.

Pia maadhimisho ya sherehe za Kitaifa husaidia kuonyesha historian a utamaduni wetu. Kupitia maadhimisho ya siku ya Mahujaji wa nchini Uganda, yanatusaidia kutambua historia ya dini ya Kikristo nchini Uganda.

Sherehe hizi ni muhimu kwa sababu yanasaidia familia kuimarika. Familia ni nguzo adhimu ya taifa husika. Wakati wa kusherehekea sherehe za Kitaifa, ofisi zote hufungwa na watu wote huenda nyumbani kwao kusherehekea na kufurahia na familia zao. Sherehe hizi zina faida chungu nzima katika jamii husika.

**MWISHO**